**Deutsche Welle Radio**
**“Learning By Ear”**
**Mafunzo na Kazi 07: Ukosefu wa Ajira**

**Mwandishi : Emmanuel Rushingabigwi, Rwanda**
**Mhariri : Sandrine Blanchard**
**Tafsiri : Anne Thomas**
**Kiswahili: Eric Ponda**

---

**1 Msimulizi-**
**3 Sauti : Albert MURANGWA (Mwakilishi wa baraza la Kitaifa la Vijana)**
**Sylvie ( Mwanamke wa Makamu)**
**Hassan (Mvulana wa Makamu)**

---

**Intro**

Hujambo na karibu kwa makala ya “Leraning by Ear”, Noa Bongo jenga maisha yako tukizungumzia mafunzo na kazi. Leo tutazungumzia maada tofauti kidogo; kuhusu ukosefu wa ajira.

Idadi ya watu wasio na ajira hasa miongoni mwa vijana inaongezeka kwa kiwango cha kutisha barani Africa..

**Music**

Kulingana na ripoti ya mwaka 2005 ya shirika la kimataifa la Leba, ukosefu wa ajira umeathiri takriban asilimia 21 ya vijana walio na kati ya umri wa miaka 15 hadi 24 barani Africa -- kiwango hiki mmoja kati ya

kila Wavulana 5 barani humu hawana ajira. Na katika nchi nyingine kama Vile Sierra Leone, zaidi ya nusu ya idadi ya vijana nchini humo hawana kazi licha kwamba wengi wao wamesoma hadi vyuo vikuu na kufuzu kwa shahada za digrii. Baadhi ya mataifa barani Africa yanajaribu kurekebisha hali hii, ambayo sio tu inaathiri kiwango cha maisha bali chumi za mataifa haya. Rwanda, kama mataifa mengine,inakabiliwa na hali ngumu ya ukosefu wa kazi. Na hata katika mataifa mengine ambayo takwimu zinaonyesha hayajaathirika sana, mikakati inabuniwa kuchunguza na kukabiliananna na hali hii . Rwanda kwa mfano imebuni baraza la kitaifa la vijana kuchunguza suala hili. Albert Murangwa ni katibu mkuu wa baraza hili la kitaifa.

**1. O-TON MURANGWA** (Kifaransa)

‘Tatizo hili ni kubwa sana hasa miongoni mwa wanafunzi wanaomaliza masomo yao ya shule za sekondari na vyuo vikuu. Imekuwa vigumu kwa wanafunzi wanaomaliza kupata kazi baada ya kumaliza masomo yao..”

Hali hali ni hiyo kwa Hassan Nyakizwanimana mwenye umri wa miaka 20, na ambaye sasa anafanya mafunzo ya utendaji kazi katika sekta ya ushonaji mjini Nyamirambo, moja wapo na wilaya yenye shughuli nyingi mjini Kigali.

**2. O-TON HASSAN 1** (Kinyarwanda)

" Baada ya miaka sita ya masomo yangu katika shule ya msingi, nilijiunga na shule ya sekondari kwa miaka miwili, lakini singeweza kuendelea na masomo zaidi kwa kuwa wazazi wangu walishindwa kunilipia karo. Maisha ni magumu hasa kwa watu wa sehemu za mashambani na ndio maana nikaamua kuja mjini Kigali kutafuta kazi.

Kila jioni Sylvie mwenye umri wa miaka 23 hukutana na marafiki zake katika moja wapo ya baa mjini Kigali. Hali yake ni tofauti kwani hakumbana na matatizo mengi kama ilivyo kwa Hassan. Yeye anatoka familia inayojiweza kidogo. Alisoma hadi chuo kikuu mjini Kigali mwaka wa 2006 na kufuzu kwa shahada ya Digrii kuhusu masuala utawala. Lakini tatizo lake ni kwamba tangu wakati huo hajafanikiwa kupata kazi.

**3. O-TON SYLVIE 1** (Kifaransa )

" Kila tuendapo tunaulizwa vyeti vyetu, tukiwapa vyeti hivyo kisha tunaambiwa tusubiri watatuita. Basi unarudi nyumbani kusubiri, lakini wapi! Hakuna mtu anayekuita "

Hassan na Sylvie wanatafuta usaidizi wa serikali kwa tatizo lao. Na kwa upande wake serikali imeahidi kupanga mikakati ya kukabiliana na hali ya ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana. Albert Murangwa ni katibu mkuu wa baraza la kitaifa la Vijana nchini humo.

**4. O-TON MURANGWA 2** (Kifaransa)

”Tumebuni sera na mipango husmeans kwa mafunzo ya taaluma mbali mbali. Mwaka huu 2008 kuna mipango ya kuwaajiri vijana ambao utaendelea hadi mwaka wa 2012. Kuna wakfu wa kuwasaidia vijana wasio na ajira utakaozinduliwa hivi karibuni na ambao utawasaidia sana vijana kupata kazi au kuanzisha biashara zao punde wanapomaliza masomo.

Mpango huu huenda utamsaidia sana Hassan. Kijana huyu ambaye anajizatiti kujifunza ushonajni, anamatumaini makubwa kwamba siku moja atafaulu.

**5. O-TON HASSAN 2** (Kinyarwanda)

”Nitaiomba serikali ianzishe mashirika ya kuwasaidia vijana wenye taaluma mbalimbali. Mwanzo wanahitaji kupewa vifaa. Kwa mfano, hebu tizama hii mashini ya kushona… inagharimu faranga 400,000 pesa za Rwanda, (karibu Euro 495) Kama tungekuwa na mashini hizi katika karakana kubwa kuliko hii, tungeweza kuchukua mikopo na kulipa polepole na hivyo kustawisha biashara yetu.. ”

Sylvia anakubalia na mawazo hayo, lakini haamini kuwa hatua hii inaweza kufaulu katika sekta zote.

**6. O-TON SYLVIE 2** (Kifaransa)

” Itategemea sekta yenyewe.Naamini kwamba kuna makundi ya vijana yanayojaribu kuanzisha biashara zao wenyewe. Kwa mfano

katika sekta ya Teknolojia ya mawasiliano,… Vijana wanaweza kuanzisha kampuni zao za kurekebisha komputa, lakini kwa hakika inategemea sekta yenyewe.

Sylvie anasema kuwa Digrii nyingine ni rahisi kupata kazi.

**7. O-TON SYLVIE 3** (Kifaransa)

”Usimamizi -- Nadhani watu wengi wanasomea masuala ya usimamizi wa kifedha, hata katika shule nilikosomea, wanafunzi wengi wamesomea masuala ya usimamizi. ”

Serikali ya Rwanda inahimiza Mtu kusomea taaluma mbali mbali ili kuongeza nafasi zao za kuajiriwa.. Albert Murangwa hasa anawahimza vijana ambao hawajasoma sana.

**8. O-TON MURANGWA 3** (Kifaransa)

”Kwa mfano vijana walioko katika sekta ya kilimo au ufugaji. Tunajaribu kutafuta njia ya kupanua taaluma za kazi ya mikono au bisahara. Nadhani kwa kufanya hivyo tunaweza kukabiliana na mahitaji yao. ”

Ingawa Sylvie, anashahada ya Digrii kuhusu masuala ya Usimamizi, na Hassan bado anajifunza kazi ya ushonaji, wote wanakabiliwa na tatizo la aina moja.. Ukosefu wa kazi…!, na wasi wasi wao mkubwa ni

kwamba hawataki kuwa mzigo kwa jamii kutokana na ukosefu wa kazi miongoni mwa vijana nchini humo.

**9. O-TON SYLVIE 4** (Kifaransa)

"Ni kweli tunajihisi kutengwa…..tunajihisi kunabaguliwa kwa sababu kama huna pesa basi unajiona mnyonge, kila wakati kuombaomba! Huwezi kuomba kila wakati kwa sababu maisha ni magumu hapa…! Hali ya maisha ni ngumu sana. Ni mbaya na hairidhishi hata kidogo……!

Hassan anakubaliana naye, anasema kuwa ukosefu wa kazi kunaathiri hali yake ya kutangamana hasa na wasichana ambao humuona mtu asiye na pesa kila mara anapojaribu kuzungumza nao.

**10. O-TON HASSAN 3** (Kinyarwanda)

"Nawezaje kumtongoza msichana nikiwa nimevalia mavazi ya aina hii? Hebu tizama shati langu lilivyoraruka…! Naweza kweli kumtongoza msichana nikiwa nimevalia hivi? Atanidharau sana au hata kunitemea mate. Labda mambo yatabadilika ikiwa na kazi na pesa niweze kuvaa vizuri..…"

Huku Hassan akiwa na matumaini kwamba siku moja atakuwa na kazi nzuri na pesa, mahitaji yake ya chakula na mavazi yataendelea kutegemea imani ya muajiri wake katika kazi hiyo ya ushonaji Sylvie

hufanya kazi zisiambatamna na kiwango chake cha elimu, kama vile kazi za usukaji nywele, ili kuepuka hali ya kumuomba pesa Dadake.

Hana budi ila kuendelea kuvumilia akitumai kuwa maisha yatabadilika na kupata kazi nzuri baadaye.

| **Muziki** |
|---|

**Outro**

Na ni hayo tuliyoweza kumuandalia kwa leo katika makala haya ya Learning by Ear kuhusu ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana wengi barani Africa .Iwapo unataka kukisikiliza tena kipindi hiki au kutoa maoni yako unaweza kutembelea mtandao wetu : www.dw-world.de/lbe Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa.